TANGAZO LA SERIKALI NA. 526 la tarehe 28/6/2024

SHERIA YA UFUGAJI NYUKI
(SURA YA 224)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 11(1))*

AMRI YA KUTANGAZA HIFADHI YA NYUKI YA TAIFA MALINGA YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Hifadhi ya Nyuki ya Taifa Malinga ya Mwaka 2024.

Tangazo

2. Eneo la ardhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Hifadhi ya Nyuki ya Taifa Malinga.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*


WILAYA YA MOMBA

HIFADHI YA NYUKI YA TAIFA MALINGA

*Makadirio ya eneo:* Hekta 761.287 au Kilometa za Mraba 7.61

Unakopatikana na Mipaka:

Eneo lote la ardhi ya mataji wazi awali chini ya Msitu wa Malinga linalopatikana Wilaya ya Momba, Mkoa wa Songwe kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 2697 ya mwaka 2016 (Skeli 1:10,000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na lenye mipaka ifuatayo:




Dodoma,
24 Mei, 2024

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*